

MRADI WA KUELIMISHA KIFUA KIKUU (TUBERCULOSIS)



MOSAIC

MOSAIC, kupitia msaada wa Wakala wa Afya ya Uma ya Canada, inafanya kazi ya kukuza ufahamu na kupunguza unyanyapaa dhidi ya kifua kikuu (TB) katika jamii zilizoko hatarini. Tunashirikiana na taasisi zinazotoa huduma ya afya, tasisi za huduma kutoa elimu na vitendea kazi - pamoja na fursa sawasawa kwa huduma na matibabu ya TB.



Public Health
Agency of Canada

Agence de la santé
publique du Canada

UHAKIKA MUHIMI KUHUSU TUBERCULOSIS(TB):

- TB ni hatari lakini ni maambukizo yanayosababishwa na virusi vinavyosambaa hewani lakini **yanayotibika na kuponyeka**.
- Kirusi cha TB kinapoingia kwenye mapafu ya mtu, kawaida mwili utakizuia kirusi kukua, na mtu hatajisia kuugua—hii inaitwa **TB iliyodumaa**. Kuna uwezekano mdogo kirusi kukua na mtu kujisia mgonjwa—hii inaitwa **TB amilifu**.
- Watu wenye **TB amilifu** wana dalili zinazojumuisha kikohozi cha muda mrefu na homa, na wanaweza kueneza kirusi cha TB kwa wengine. Watahitaji uangalizi wa matibabu.
- Watu wenye **TB iliyodumaa** hawana dalili zo zote, hawajisikii kuumwa, na hawawezi kueneza kirusi cha TB kwa wenzao.
- Kuna watu wengi duniani wanaoishi na **TB iliyodumaa** bila kujifahamu.
- Kuna uwezekano mdogo wa **TB iliyodumaa** kustawi kuwa **TB amilifu** baada ya muda. Ni muhimu kuzuia TB amilifu kwa kufanya vipimo na kutibu **TB iliyodumaa** – kipimo cha TB cha ngozi kinaweza kusaidia kugundua kama mtu anayo **TB iliyodumaa** au hana.
- Muda wa matibabu ya **TB iliyodumaa** unategemea aina ya dawa na inaweza kuchukua kati ya miezi 3 hadi 9.
- Katika British Columbia, vipimo na matibabu ya TB ni bure kwa watu ambao wako hatarini.

- Hakuna aibu kupimwa ukawa na **TB iliyodumaa**, na watu wasiwe na hofu ya kufanyiwa uchunguzi.
- Ye yote anaweza kupimwa na kukutwa na TB bila kujali kabila, jamii, utamaduni, dini, kiwango cha elimu, kazi, hadhi ya uhamiaji, hadhi ya kijamii na kiuchumi, na mwelekeo wa kijinsia.
- Kuwa na **TB iliyodumaa** haiathiri kipengele cho chote cha utaratibu wa kawaida wa shughuli za kila siku. Mtu mwenye **TB iliyodumaa** anaweza kuendeleza mahusiano, kwenda kazini, kuhudhuria shule, na kubakia kushiriki kikamilifu katika jamii bila ya kujisikia mgonjwa, na bila ya hofu ya kueneza maambakizo kwa wengine.
- Mtu mwenye **TB iliyodumaa** hawahitaji kuondolewa kwenye jamii au kutengwa na familia, marafiki, na jamii.
- Kukutwa na **TB iliyodumaa** hakuathiri hadhi ya uhamiaji, au kuthibiti usafiri wa ndani na nje ya nchi.
- Katika Canada, taarifa za afya **zinatunzwa na kulindwa** kwa siri madhubuti kupitia sheria za serikali ya Shirikisho na Jimbo.
- Katika Canada, upimaji na utabibu wa **TB iliyodumaa** ni wa hiari na unafanywa ili kuzuia ugonjwa wa **TB amilifu**. Kuzuia **TB**, wasiliana na mtoaji/watoaji huduma ya afya au kliniki za TB.

KLINIKI ZA UCHUNGUZI WA TB KATIKA JIJI LA VANCOUVER:

VANCOUVER

655 West 12th Avenue

Vancouver

Simu: 604-707-2692

MASAA YA KAZI:

Jumatatu, Jumanne, Jumatano,

Ijumaa: 8:00 AM - 4:00 PM

Alhamisi: 9:30 AM - 4:00 PM

NEW WESTMINSTER

100 - 237 E. Columbia Street

New Westminster

Simu: 604-707-2698

MASAA YA KAZI:

Jumatatu, Jumanne, Jumatano,

Ijumaa: 8:00 AM - 4:00 PM

Alhamisi: 9:30 AM - 4:00 PM

NYENZO ZA ZIADA

TAARIFA ZA AFYA

- **Kiunganisho cha Afya BC** – piga **811** simu ya bure (huduma za kutafsiri zinapatikana kwa lugha Zaidi ya 130) au tembelea www.healthlinkbc.ca/healthlinkbc-files/tuberculosis
- **BC CDC** - www.bccdc.ca/health-info/diseases-conditions/tuberculosis

HUDUMA ZA LUGHA: Unaweza kupata huduma za kutafsiri kupitia **Huduma za Lugha za Jimbo la BC (BC Provincial Language Services)**. Unapokuwa unawasiliana na wahudumu wa afya au kliniki za TB, ulizia huduma hii, au wasiliana na jumuiya au taasisi za makazi kwa msaada zaidi.

HUDUMA ZA JUMUIYA NA MAKAZI:

MOSAIC na jumuiya nyingine za makazi zinatoa utegemeo kwa jumuiya zote mbali mbali aina za huduma zikiwemo afya/ustawi, ajira, makazi, lugha, kulea watoto na programu za familia katika sehemu mbali mbali. Kama unahitaji huduma au msaada, wasiliana na MOSAIC kwa taarifa Zaidi.

MOSAIC HEADQUARTERS

5575 Boundary Road

Vancouver

Simu: 604 254 9626

Barua pepe: info@mosaicbc.org

Utambuzi: Yaliyomo katika broshua hii yanatokana ushariano wa jumuiya, pamoja na rasilimali kutoka Kitengo cha Kudhibiti Maradhi cha BC, Mamlaka ya Huduma za Afya ya Jimbo, na Wizara ya Afya ya BC. Mradi huu umefdhiliwa kwa ukarimu wa Wakala wa Afya kwa Umma ya Canada.